
# Our MULTILINGUAL VOICES

Masika 2021 www.houstonisd.com/voices Toleo la I Chapa ya 3

## TONE LA BUSARA



Geovanny J. Ponce

Wazazi wote wanaweza kuchangia katika elimu ya watoto wao kwa njia anuwai, hasa katika majira haya. Uhusika wa wazazi na msaada wao ni muhimu sana wanafunzi wanapojitahidi kukuza lugha ya pili na ujuzi wa kimasomo. Wazazi wanaweza kusaidia watoto wao kiakademia kwa kuchangia maendeleo ya mwanafunzi katika lugha ya Kiingereza na ujuzi wa kiakademia nyumbani. Tumia mikondo ifuatayo kumsaidia mtoto wako kufuzu kiakademia, sio kwa lugha moja tu bali kadhaa:

- Endelea kukuza ujuzi wa kimasomo wa mtoto wako kwa lugha ya kwanza nyumbani huku ukijenga na kufanya mazoezi ya Kiingereza na maudhui ya kiakademia.
- Msihi mwanao kusimulia na kuandika hadithi nyumbani kwa Kiingereza au lugha yao ya mama. Kuwa na nafasi ya kumuuliza mwanao maswali kuhusu hali mbalimbali ili kumwezesha kupata maana na kuweka mazoea yanayofaa ya lugha hiyo mpya.
- Kuwa na wakati uliotengwa wa kusoma ambao wewe na mwanao mnaweza kuufuata. Hili litakuwa na mchango mkubwa sana kwa wakati unaotumika kuzoea lugha hiyo na maudhui.
- Soma na mwanao mara kwa mara. Waruhusu waweze kutangamana na aina tofauti za makala ya kusoma ikiwemo mtandaoni na vitabu-sikizi.
- Kuwa na uhusiano mzuri na shule ya mwanao. Wasiliana na mwalimu wa mwanao kila mara. Mwanao au famila yako iwapo na vizuio kwa elimu ya mwanao, chuo kinaweza kukuunganisha wewe au mwanao kwa rasilimali zinazofaa kuhakikishia kufuzu kwa mtoto huyo kiakademia.

Wazazi, walimu na shule, pamoja wanaweza kusaidia wanafunzi kufikia upeo wa uwezo wao.

**Geovanny J. Ponce**
**Msimamizi wa eneo la Shule za Mashariki**

## UJUMBE KWA WAZAZI ...

# Msukumo wa Benjamin Kufuzu

**Benjamin Estefano Diaz Villa alikuwa na umri wa miaka 7 tu wazazi wake, wote wenye kufuzu na shahada ya uhandisi, walipoanza maisha mapya Marekani kufuata maisha bora kwa Imani. Safari ya familia hiyo ilianza walipotoka walipozaliwa, huko Medellin, Colombia mwaka 2006. Diaz anayakumbuka masaibu aliyopitia shuleni kwa kuwa mzungumzaji ambaye ni mzawa wa Kihispania:**

*Lililokuwa gumu kwangu ilikuwa kuelewa lolote ambalo halikuwa linahusiana na sayansi au hisabati. Kwenye fasihi na historia yangu, nilikuwa niking'ang'ana sana kufanya vyema kwa sababu ya ujuzi wabgu pungufu wa Kiingereza. Hayo mengine yote yalikuwa murwa kwangu.*

**Je, "waraka kwangu" yako ingekuwa ipi, ulipokuwa na umri wa miaka 9 kuhusu masomo?**
*Ningejiambia kulenga kwenye nidhamu na azma-binafsi, tabia hizi zitasaidia kufanya vyema na kukuza zaidi maeneo ya mahitaji-sifa hizi zitakusaidia kufuzu! Ningejikumbusha kutumia fahamu yangu ya kiufundi kuelewa maeneo mengine ya kiisimu kama fasihi, kusoma na kuandika. Hali kadhalika, hivyo ndivyo nilifaulu kwa kufanya vyema zaidi kwa masomo yangu yasiyo ya uhandisi.*

**Ujumbe wa Benjamin kwa walimu wa HISD ni huu:**
*Wanafunzi wahamiaji, kama mimi, kwenye madarasa yenu, wanafunzu wanaofuzu kwenye lugha za jumla za hisabati, mantiki na Sayansi. Mnapowafunza kusoma na kuandika, linganisheni sheria za uandishi na zile za Hisabati au Sayansi, "fomula" ambazo haziwezi kuvunjwa. Vilevile wanafanya vyema wanapopewa hati na dondoo za kukariri kwa moyo. Kwa kuwapa vyenzo vya kujifunza, baada ya muda wanafunzi hawa wataanza kujiuliza swali la mbona iwe hivyo. Hapo ndipo ujuzi wao wa kuhakiki utazoezwa na uandishi wa insha za uhakiki unaweza kufunzwa.*

**Tueleze kuhusu kufaulu kwako kwenye Chuo cha Houston na kufaulu kwako unakutabaruku kwa nini?**
*Kufaulu kwangu nakutabaruku kwa Mungu, Familia, jamii ya kanisa, walimu wazuri, shule nzuri, na program nzuri akademia ya Chuo cha Houston. Mungu ameniruhusu kuwa na wazazi ambao walinifundisha umuhimu wa elimu na kufanya vyema. Kupitia mwelekezo wa Mungu nimeweza kufaulu kiakademia na kwa baraka zake nimeweza kupata ufadhili wa kiakademia. Mwishowe, kuwa katika utendaji wa huduma kwenye kanisa lililoniruhusu kufanya vyema kabisa kama mwanafunzi wa chuoni. Hili linaweza kukosa kuwa na maana lakini ni kweli. Mtu anaweza kudhani kuwa kuwa mwanafunzi mzuri unahitaji kusoma na kuangazia kazi anayoifanya tu. Hilo ni kweli kwa 25% pekee. Yaliyobaki yanahusiana na ubinadamu mtu anaweza kuwa nao. Kuwa mtu wa kidini kuhusiana na maisha ya kiroho, hisia na afya ya kimwili huchangia katika kufaulu kwa mtu huyo.*



**Benjamin Estefano Diaz Villa ameteuliwa kama Mwanafunzi Mkuu wa Chuo wa Mwaka katika Chuo cha Houston 2020-2021**

**Ungesema wazazi wako wamechangia vipi katika kufaulu kwao?**
Ningejumuisha uhusika wa wazazi wangu kwa kufaulu kwangu kwa kusema:

Wote walikuwa wahandisi ambao waliamua baadaye kuenda kwenye seminari na kufuzu na vyeti vya uzamili na uzamifu katika huduma ili kufanya kazi ya injili na kueneza ujumbe mwema wa Mungu. Pande zao zote za maisha za uhandisi na huduma zimenifunza umuhimu wa elimu na kazi ya kitaaluma na umuhimu wa kuwa katika mkondo alionipangia Mungu na wale walio karibu nami. Wazazi wangu wangechagua kuendelea na kazi zao za uhandisi na kujenga maisha ya kifahari, lakini waliamua kufuata mkondo uliopangwa na Mungu. Na hiyo ndiyo imani ningetaka kuwa nayo katika mabadiliko ya maisha.

Benjamin alihudhuria Shule ya Msingi ya Jean Hines Caldwell na Shule ya Msingi ya Brookline kabla ya kuhudhuria Shule ya Kati ya Rice. Hatimaye alifuzu kutoka kwa Shule ya Sekondari ya DeBakey ya Taaluma za Afya.



*(imeendelezwa nyuma)*

## UJUMBE KWA WAZAZI ...

*(imeendelezwa kutoka mbele)*

Mafanikio ya Benjamin Kiakademia yanahusu yafuatayo:

- **2018 Adhama ya Chuo Mwanafunzi Bora Mwaka wa Kwanza**
- **2020-21 Mwanafunzi Mkuu Bora – Chuo Kikuu cha Houston, chuo cha Cullen cha Uhandisi,**
- **2019-20 Mwanafunzi Mkuu Bora – Chuo Kikuu cha Houston, chuo cha Cullen cha Uhandisi,**

Miongoni mwa hizi tuzo mbalimbali, Diaz Villa amepata mafanikio ya muhimu- kufaulu kuwa raiya wa Marekani. Upeo wa kijana huyu wafikia ule wa nyota, azma yake ni pamoja na kupata uzamifu katika Uhandisi wa anga ya nje.

KusomazaidikuhususafariyakufuzuyakiakademiayaBenjamin,bonyezakiungokifuatacho: ***https://www.egr.uh.edu/news/202101/diaz-villa-honored-year%E2%80%99s-outstanding-senior***

### Maneno ya Kutia Moyo kutoka kwa mzazi wa Benjamin

**Je, ushauri wako kwa wazazi wa watoto wanaojifundisha Kiingereza ni upi?**
*Wapende watoto wako na uwasaidie kuazimia mustakabali wao. Wafuatilie na hawatawahi kuwa wapweke, kwa kuwa Mungu atakuwa nao, popote walipo, wakiwa shuleni, chuoni, kanisani, dukani au kwenye vituo vyao vya kazi. Wasaidie na uwahimize watoto wako kufaulu na uwe wakili wao mkuu.*

**Ulimuhimiza Benjamin vipi alipokuwa aking'ang'ana kujifundisha Kiingereza?**
*Wazazi wa Benjamin wangesoma hadithi ya Kiingereza na kuisimulia hadithi hiyo kwa Kihispania. Hili lilimruhusu kukumbuka hadithi na kumpa wakati zaidi kuangazia misamiati ya kiakademia.*

**Ungewapa wasia upi wazazi wasiozungumza Kiingereza lakini wangependa kuwasihi watoto kujifundisha kadri wawezavyo?**
*Tungewashauri wazazi kuchukua wakati kuwafunza watoto wao lugha zao asili. Kuwa kielelezo kwa kuchukua wakati wako kusoma, kuandika, na kuchora na vilevile kutazama program za televisheni mwigo, ili pamoja mujifundishe kuelewa. Kwa jumla, wakumbushe watoto wako kila mara kuwa unawapenda na kuna mipango ya maisha inayowasubiri.*

Kutoka kwa Aprili 15, 2021 kutoka ***https://www.egr.uh.edu/news/202101/diaz-villa-honored-year%E2%80%99s-outstanding-senior*** ■

## KURUNZI YA BURNET ES

Shule ya Msingi ya David G. Burnet inapatikana kwenye Upande wa Mashariki na ndicho chuo pekee chenye programu ya Uwili Lugha ya Vanguard kwa wanafunzi wa East End katika mfumo wa 50/50 Two-way Immersion. Kutoka mwanzo wake mwaka 1926, Shule ya msingi ya Burnet imeendelea kujitahidi kuauni elimu bora iwezekanavyo kwa wanafunzi wake wote. Leo, Shule ya msingi ya Burnet ina zaidi ya wanafunzi 500 katika programu yao ya Uwili Lugha na ina misheni ya kutoa programu sanifu ya elimu kupitia ujuzi wa kutatua matatizo wakati wote wakiumba mahusiano mazuri na kuyakuza.



**Familia ikifurahia Usiku wa Sayansi katika Shule ya msingi ya Burnet.**

Kupitia uongozi wa Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi ya Burnet, Bi. Ana Cantu, uhusiano imara wa wazazi/jamii baina ya nymbani na shule umestawishwa. Wazazi wanahimizwa kujumuika katika elimu ya mtoto wao kwa kuwa washirika badala ya wahusika wa mbali. Wazazi ni mojawapo ya funguo katika kufaulu kwa mtoto wao na wanaweza mara nyingine kuonekana shuleni wakihusika na matukio ya wanafunzi, kahawa na mwalimu mkuu au masomo ya kuwakuza kitaaluma wazazi ili kumsaidia mwanafunzi kusoma nyumbani. Mwalimu Mkuu anaamini kuwa wazazi ni washirika na uhusika wao utasaidia kujifundisha kwa wanafunzi wao.

Wanafunzi wanapenda kuhudhuria Shule ya Msingi ya Burnet na kiwango cha 97% cha mahudhurio kinaonyesha furaha yao katika kujifundisha. Wanafunzi wanahimizwa kuhudhuria na kuwa wahusika amilifukatika masomo. Ukitembea katika kumbi za Shule ya Msingi ya Burnet unaweza kusikia wakikariri maneno kwa kasi, wakihesabu, wakijadiliana kuhusu mada tofauti, kusoma kwa nguvu na kumalizia miradi katika maeneo ya maudhui mbalimbali.

Kama ungetaka kujua Zaidi kuhusu Shule ya msingi ya Burnet au program za akademia tafadhali zuru tovuti yao, twitter, au akaunti ya Facebook kwa anwani zifuatazo.

***https://twitter.com/BurnetES*** | ***https://www.facebook.com/davidg.burnet.37/***

***https://www.houstonisd.org/burnetes*** | Barua pepe: ***BurnetES@houstonisd.org***

Mwalimu Mkuu: **Ana Cantu**, Barua pepe: ***ACANTU5@houstonisd.org*** ■

## PROGRAMU YA KIANGAZI

HISD SUMMER SPARK
IGNITING ACADEMIC EXCELLENCE

Programu ya Kiangazi ya mwaka 2021 ni ya wanafunzi wa vidato PK-12 waliojisajili kufikia siku ya mwisho ya shule kwenye shule ya HISD na wanahitaji kufikia kiwango cha kupandishwa cheo. Programu hizi za kiangazi zinaratibiwa katika kiwango cha wilaya, zinazopangwa kwenye kiwango cha chuo, na kuwekwa maalum kukidhi mahitaji ya wanafunzi binafsi. Wakati unaoongezwa na programu za kiangazi unawapa wanafunzi nafasi nyongeza zilizojaa maelekezo na kutilia mkazo ili kufikia matarajio ya mwakani ya shule. Ni lengo la HISD kuwa kupitia program faafu za kiangazi, wanafunzi wote wanaohitaji wakati huu wa ziada watafikia viwango vinavyohitajika kupandishwa cheo, kuwa tayari kufuzu kwenye kidato kinachofuata, na kuwa kwenye mkondo wa kufuzu na wenzao wa rika lao. Bonyeza kiungo kupata maelezo ya jinsi ya kujisajili:

***https://www.houstonisd.org/Page/187497***.
**Kama una maswali kuhusu usaidizi wa kimaeneo wa mwanao wakati wa misaada ya Mwaka wa Shule Uliorefushwa (Extended School Year-ESY), tafadhali mfahamishe Msimamizi Mkuu wa Eneo au wa Misaada ya Elimu Spesheli.** ■

## KUSAIDIA WANAFUNZI WA KIINGEREZA HAPA TX

### Usaidizi wa Houston ISD

Kozi Kuu:
***https://bit.ly/3thXK9M***
Ujumbe kuhusu mafunzo ya nyumbani na HISD

Orodha ya makazi ya Kifasihi:
***https://www.houstonisd.org/Page/184314***

### Nyenzo za Wazazi

Usaidizi wa Wakala wa Elimu Texas:
***http://bit.ly/3t69k8k*** ■

## FEDHA ZA ARP ACT ESSER III

### Toa marejeo yako ya Jinsi ya Kutumia Fedha Inavyofaa

HISD inakusanya ujumbe wa ziada kutoka kwa wazazi wa wanafunzi ambao ni wanaojifundisha lugha ya Kiingereza, wasio na makazi, na/au wanafunzi walio na ulemavu jinsi ya kutumia fedha za ESSER III. Uchunguzi huu umegawanywa kwa vipande viwili. Sehemu ya (1) ESSER III- Matumizi ya Fedha inavyoruhusiwa/ Shughuli, ambazo huhitaji wazazi kutoa maoni kuhusu jinsi ya kuzitumia fedha hizo vyema na Sehemu ya (2) Urudishaji wa ufundishaji wa ana kwa ana, ambao huhitaji wazazi kutoa maoni kuhusu wakati wa shughuli zilizolengwa kwa wanafunzi kurudi kusoma ana kwa ana. Kama ushakamilisha uchunguzi tafadhali upuuze. ***https://bit.ly/3oZ8fO6*** ■

## UFADHILI WA WAKIMBIZI 2021

YMCA International Services inapeana misaada ya kifedha kwa wanafunzi wa wakati-wote wa vyuo vikuu wenye ni:

**wakimbizi | waliothibitishwa
kuhifadhiwa walio na Visa spesheli za uhamiaji wahasiriwa wa usafirishaji haramu wa binadamu.**



Wanafunzi wote wanapaswa wajaze ombi wakieleza kuhusu usuli wao wa kiakademia na wa kibinafsi. Wanafunzi wanaambiwa wawasilishe insha mbili ili kuzingatiwa kwa ufadhili. Washindi watateuliwa kulingana na mahitaji na mafanikio.

**Maombi yanakubalika kuanzia Aprili 1- Juni 18**
Pata ombi: ***Shorturl.at/alyPS*** | Unganisha kwenye kipeperushi: ***https://bit.ly/2R3Jl2F*** ■